

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA MANISPAA YA MTWARA - MIKINDANI



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. MM/MC/PF/L1/8/152

Tarehe: 24/05/2022

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani anawatangazia waombaji wote wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani kuleta maombi ya kazi kwa nafasi iliyoainishwa hapo chini, baada ya kupata idhini ya kutekeleza Ikama na Bajeti kwa Ajira mpya katika mwaka wa fedha 2021/2022 kwa barua yenye Kumb. Na.FA.97/228/01/9 ya tarehe 13 Mei, 2022, kutoka kwa Katibu Mkuu UTUMISHI, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Hivyo basi Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa wataanzania wote wenye sifa kuomba nafasi ifuatayo:-

**1.KATIBU MAHSUSI DARAJA LA III NAFASI (03)**

**i. Sifa za kitaaluma za mwombaji.**

- a) Awe amehitimu Elimu ya Kidato cha Nne (IV)
- b) Awe amepata mafunzo ya Uhazili na kufaulu mihani wa Hatua ya tatu. Awe amefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kiingereza maneno 80 kwa dakika moja na awe amepata mafunzo ya Kompyuta kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti katika Programu za Windows, Microsoft Office, Internet, E-mail na Publisher.

**ii. Mshahara.**

Ngazi ya mshahara TGS B

**iii. MAJUKUMU YA KATIBU MAHSUSI DARAJA LA III**

- a) Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida.
- b) Kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao, na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
- c) Kusaidia kutunza kumbukumbu / taarifa za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba ya kazi zingine zilizopangwa kutekelezwa katika ofisi anamofanyia kazi na kumuarifu Mkuu wake kwa wakati unaohitajika.
- d) Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo ofisini.
- e) Kusaidia kufikisha maelekezo ya Mkuu wake wa kazi kwa wasaidizi wake na pia kumuarifu kuhusu taarifa zozote anazokuwa amepewa na wasaidizi hao.

- f) Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa Maofisa walio katika sehemu alipo, na kuyakusanya , kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika
- g) Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na Msimamizi wake wa kazi

## **2. MASHARTI YA JUMLA**

- i) Waombaji wawe ni raia wa Tanzania mwenye umri kati ya miaka 18 na usizidi 45.
- ii) Waombaji wawasilishe picha mbili za hivi karibuni.
- iii) Waombaji wawasilishe maelezo binafsi (Curriculum Vitae) yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini watatu (Referees) wa kuaminika.
- iv) Waombaji waambatanishe nakala ya vyeti vya masomo na taaluma,
- v) Cheti cha kuzaliwa. Muombaji atakayewasilisha “Result slip” “statement of results” “Provisional results” au “Transcript”. Maombi yake hayatapokelewa
- vi) Kwa waliosoma nje ya nchi elimu ya kidato cha nne na kidato cha sita wawasilishe uthibitisho kutoka Baraza la Mitahani la Tanzania (NECTA).
- vii) Kwa waliomaliza vyuo nje ya nchi wawasilishe uthibitisho kutoka Tume ya Vyuo Vikuu (TCU).
- viii) Waombaji waandike namba ya NIDA katika barua ya maombi au waambatishe nakala ya Kitambulisho cha Uraia (National Identification Number) kutoka Mamlaka ya vitambulisho (NIDA)
- ix) Waombaji watakaokidhi sifa zinazotakiwa ndio pekee watakaoitwa katika usaili..
- x) **Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe 06/06/2022., saa 9:30 Alasiri.**

**MUHIMU:** Kumbuka kuambatanisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu na nyaraka zote zinazohitajika. Maombi yote yatumwe kwa njia ya posta kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi wa Manispaa,  
S.L.P 92,

**MTWARA-MIKINDANI**

Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya Halmashauri  
[www.mtwaramikindanimc.go.tz](http://www.mtwaramikindanimc.go.tz) .

Tangazo hili limetolewa na:-



COL Emanuel H. Mwaigobeko  
**MKURUGENZI WA MANISPAA**  
**MTWARA-MIKINDANI**

Kiwanja Na 168 na 171 Kitalu "K" Chikongola, Makutano ya Barabara ya Tanu na Chikongola, S.L.P 92,  
Mtwara. Simu: +255 232333102, Nukushi +255 23 2334794  
Baruapepe: md@mtwaramikindanimc.go.tz Tovuti: www.mtwaramikindanimc.go.tz